

**TUNALO JUKUMU LA KUITUNZA IMANI TAKATIFU
HADI KRISTO YESU ATAKAPORUDI MARA YA PILI
MAANDIKO: LUK 18:1-8.**

1. UTANGULIZI:

Swali hili muhimu sana la Bwana Yesu kwa wanafunzi wake linaonyesha wazi kwamba “kwa kadri kurejea kwake kunavyokaribia, uovu nao ndivyo unavyozidi kutawala, na kadri uovu unavyozidi kutawala, ndivyo watu wengi mno wa Mungu wanavyoiacha imani ya kweli. **Math 24:9-13,24-25**

- Swali hili kuu la Bwana Yesu lilikuwa pia linatoa **jukumu** kubwa kwa wanafunzi ili wawe tayari kabisa tena kwa hali yoyote ile **kuitunza imani** ya kweli hata katikati ya manabii wa uongo na makristo wa uongo wengi watakaoibuka katikati yao; maana hata Malaika walioshindwa kuitunza (kuilinda enzi yao Mungu aliwatema. **Yuda 1:3-6**

2. Manabii wa Uongo na makristo wa uongo hivi sasa wanavuruga sana imani ya kweli (imani halisi) na udhihirisho halisi wa nguvu za Mungu kwa watu tayari umeanza kupotea/kufukiwa na madhihirisho bandia. 1Tim 3:8 na ndiyo sababu mtume Paulo alikuwa mkali sana kwa lengo la kulinda watoto wake wa kiroho na hawa manabii wa uongo na makristo wa uongo. **Gal 1:9.**

- Leo hii Manabii wengi wa uongo wameongezeka sana, na kwa mujibu wa neno la Mungu, wataendelea kufanya ishara nyingi na kubwa mno- (**Math 24:24-25**) na wale wote wasio na msingi imara wa neno la Mungu ndani yao, upepo huu wa miujiza kwa vyovyote vile lazima **utawazoa** na kuwatoa kabisa kwenye imani ya kweli.
- **Eneo ambalo nimejifunza sana katika maisha yangu ya Utumishi ni hili kwamba waumini (wakristo) wengi kwa sasa hawapo tayari kuishi kwa kupata mateso (kuteseka) kwanza kwa ajili ya Kristo na kulitii Neno**

lake kama sehemu ya imani ya Kikristo!!. *Yoh. 15:20. Math. 5:10-12, Mdo. 14:21-22 na 2Timo. 3:12.* **Badala yake Ukristo umechukuliwa kama eneo la kuwa na maisha mazuri na mafanikio ya haraka!!** Ni sawa na vijana wengi wanavyotaka maisha ya hali ya juu kwa muda mfupi tu pindi wanapomaliza masomo/wanapoanza kazi!!

- Dalili hii aliyoisema Yesu Kristo kwa sasa inatimia sana tena sana. **Math 24:4-5.** Manabii wa uongo na makristo wa uongo wanatumia jina la Yesu!! Hii ni mbinu hatari sana na ambayo **inapumbaza** na **kudanganya** wengi wasiokuwa na **ufahamu** wa kutosha wa Neno la Mungu, na eneo la kudanganya ndugu zangu **shetani ni mtaalamu na mbobezi, ni taaluma yake kabisa tangu zamani.** *Math. 24:11, Mwaz. 3:1-6, Yoh. 8:44*
- 3. Turudi kwenye swali la msingi la Bwana wetu Yesu Kriso **“Walakini atakapokuja mwana wa Adamu je ataiona imani duniani?”**
 - Kuishi maisha matakatifu katika dunia hii ya sasa kunahitaji **kujikana** sana, wateule wengi **wamesongwa** sana na maisha haya kiasi cha kusahau kwamba Yesu atakaporudi yote haya wanayoyasumbukia yatakuwa hayana maana tena; Wateule wengi hawana muda wa kutosha wa kuomba (kuwa na uhusiano wa karibu), hawana muda wa kusoma na kutafakari Neno lake ili Bwana aweze kusema nao na kuwajulisha yawapasayo; Hata tumefikia mahala pa kumwonea aibu Yesu wetu na kutomtaja katikati ya waovu!! **Math. 10:32-33**
 - Swala la kutunza utakatifu ni swala la mtu binafsi, swala la kushindania imani hii takatifu ni swala la mtu binafsi **Yud1:3-4** na **1Yoh 5:18** na dhahaka zitaendelea sana kwa wanaosimamia imani kwamba umepata nini tangu ulipokaza msimamo wako kuliko sisi. **2Petr 3:3-4** na wengine wataenda mbali zaidi na kudanganya wengi kwamba Yesu hatarudi mara ya pili!! **Ni uwezo alio nao mteule ndani ya moyo ndiyo utakaomwezesha kusimamia**

imani hii takatifu aliyokabidhiwa mara moja tuu hata kama itamlazimu kufanya maamuzi magumu pindi inapobidi ili kuwapinga manabii wa uongo. 1Waf1 22:16-28

- Ukitaka kulinda imani hii takatifu lazima kabisa kuepuka lugha inayotawala sasa hivi ambayo ni udanganyifu mkubwa wa shetani kwamba lazima **uchukuliane na wenye dhambi kwa kutumia hekima za kibinadamu!! Sema kweli kama Mikaya hata kama wengine wamepatana kwa faida ya matumbo yao na Mungu muhukumu wa haki atakaporudi ataamua kwa haki.**
- Mungu sio dhalimu ndugu zangu, Kama wengine kwa kuishindania imani hii takatifu walipata mateso na kuuawa kikatili sana- **(Ebr 11:32-40)** leo ataruhusuje watu wanaochanganya changanyo imani na maovu nao wawe warithi pamoja na wale walioilinda imani na kutojichanganya kwa gharama zozote!! Siku inakuja ambayo neno hili litatimia kabisa. **Math 7:15-23. Amina**

Na

Askofu Dr. L. M. Mwizarubi

October 2021